# U B A T I Z O

# K W A

# M A J I

## JE, MUUNDO AU KANUNI YAKE UNAFANYA TAFAUTI YO YOTE?

Je, inaleta tofauti yoyote kutokana na Biblia inavyosema juu ya ubatizo wa maji katika jina la Yesu Kristo? Maoni ni mengi. Karibu kila mtu ana mawazo ya kuchangia wakati kunapotokea majadiliano juu ya ubatizo wa Kikristo. Baadhi wanabisha kukubali na wengine hupinga swala la kwamba mtu abatizwe kwa kunyunyuziwa maji au kwa kuzamishwa majini na kama abatizwe katika vyeo Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu au katika jina la Yesu Kristo. Ni wachache tu hivi karibuni wameuliza swali, "Je, huleta tofauti yo yote?"

Maoni yetu ki-ukweli hayafai, mawazo ya mtu mmoja ni mazuri kama ya mtu mwingine. Kipengele pekee katika kuamua ukweli ni Neno la Mungu - Biblia. Inasema nini juu ya muundo na kanuni ya ubatizo wa Mkristo?

## UMUHIMU WA UBATIZO

Ubatizo wa Kikristo mwanzo wake ni katika utendaji wa Kiyahudi nyakati za kabla ya Ukristo. Waliobadili kuingia katika Uyuda walibatizwa kuonyesha imani yao kwa Yehova Mungu. Wakati Yohana Mbatizaji alipotokea na kuandaa mioyo ya Wayahudi ili kumpokea Masihi wao, alidai toba, maungamo ya dhambi, na ubatizo katika maji. Alitamka "Katika tendo ninakubatiza kwa maji katika toba: Lakini yeye ajaye nyuma yangu ...atawabatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa moto" (Mathayo 3:11).

Yesu mwenyewe alibatizwa na Yohana (Mathayo 3:16). Baada ya hili, yeye na wanafunzi wake walibatiza makundi makubwa ya waamini (Yohana 3:22; 4:1-2). Alihusisha ubatizo kama sehemu ya kuzinduliwa kwa mwamini katika kanisa analoanza (Marko 16:16).

Baada ya kufufuka kwake, aliwaelekeza wanafunzi wake "Enendeni.... mkawafanye mataifa kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana na Roho Mtakatifu" (Mathayo 28:19). Kabla ya kupaa, alikutana na wanafunzi wake na "akawafunulia akili zao..., ili wapate kuelewa na maandiko, na akawaambia, Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa, na kufufuka siku ya tatu, na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi,kuanzia tangu Yerusalemu" (Luka 24:45-47).

Kwa hiyo, jukumu la kuiendeleza huduma yake, kuikuza Injili, na kustawisha kanisa la Agano Jipya juu ya wale wanafunzi wachache.

Wakiwa na ufahamu wao umefunguliwa katika mapenzi ya Mungu kulingana na mpango wa ukombozi, walijazwa Roho Mtakatifu siku ile ya Pentekoste, ambapo ilizidi kuweka nuru katika akili zao. Wakati kundi kubwa lililokuwa na shauku kuona tukio hilo la kihistoria pale Yerusalemu, Petro alihubiri ujumbe ambao uliwachoma kwa sababu ya dhambi zao. Waliwauliza mitume, "Tutendeje" (Matendo 2:37).

Jibu la Petro lilikuwa wazi bila kosa. "Tubuni, mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu" (Matendo 2:38). Kwa ufahamu wa

kiroho ambao Petro alipokea aliweza kufahamu kuwa kuzaliwa upya kulihusisha ubatizo wa maji na Roho (Yohana 3:5), kwamba Mungu alichagua unganisho la jina na maji kwa ajili ya ondoleo la dhambi, na kwamba Bwana alikusudia jina lake litajwe katika tendo la ubatizo.

Hivyo hivyo, Anania alimwambia Paulo, "simama na ubatizwe, ukaoshwe dhambi zako ukiliitia jina lake (Matendo 22:16).

**MUUNDO WA UBATIZO**

Namna au mfumo wa ubatizo wa maji ni kwa kuzamisha. Neno "Ubatizo" limetokana na Kigiriki "baptizo" linalomaanisha "kutosa, kuzamisha", Matukio yote ya ubatizo katika maandiko yanaunga mkono hali hii. Hebu tuangalie haya: "Yohana naye alikuwa akibatiza huko Ainoni ... kwa sababu kulikuwa na maji tele" (Yohana 3:23). Wakati Yesu alipobatizwa na Yohana, "alipanda kutoka majini" (Mathayo 3:16). Na yule Towashi wa Kushi na Filipo "Wakatelemka wote majini,... naye akambatiza” (Matendo 8:38).

**KANUNI YA UBATIZO**

Biblia inatupa maelekezo maalumu ya kutambua matumizi ya ubatizo wa maji, na Mungu anataka kila mtu akubaliane nao.

Mtume Paulo aliamuru, "Lolote mfanyapo kwa neno au kwa tendo fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu" (Wakolosai 3:17). Hakika maelekezo haya yanahusu ubatizo wa maji.

Wale Mitume walifahamu maana halisi ya mafundisho ya Yesu kuhusu ubatizo na waliyachukua kwa usahihi. Walielewa umoja wa jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu jina ambalo linaonyesha ukamilifu wa Uungu ni Yesu. (Ona Mathayo 1:21; Yohana 5:43; 14:26; Wakolosai 2:9.) Kila tukio walitumia au matumizi ya jina la Yesu Kristo katika ubatizo. (Angalia Matendo 2:38; 8:16; 10:48; 19:5; 22:16.) Ni dhahiri kwamba walilitaja jina lake katika tendo la ubatizo. Jina la Yesu linatambulisha na kukamilisha ubatizo kama vile jina linalowekwa katika hundi linavyokamilisha hundi hiyo.

Hatuwezi kuacha vile vipengele vya umuhimu wa ubatizo wa Kikristo, lakini lazima tutekeleze Matendo 4:12. "Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo".

Kweli, baadhi ya madhehebu yamekuwa na desturi ya kunyunyizia badala ya kuzamisha na kwa makosa walibadilisha matumizi ya vyeo hivi Baba, Mwana na Roho Mtakatifu kwa matumizi ya jina halisi Yesu. Lakini wale waaminifu watathamini kweli kuliko mapokeo na watatii mafundisho ya Injili "Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu...."

http://www.sayadi-al-nas.com

**Chapishwa na:**
**United Pentecostal Church of Tanzania**
**SLP 1271**
**Moshi, Tanzania**